

Mwenendo wa Kikristo

“Tumeitwa tuwe watu watawa wanaofikiri na kujisikia, na kutenda kwa kufuatana na sheria za mbinguni. Ili Roho aumbe upya tabia ya Bwana wetu ndani yetu tunajihusisha tu katika mambo ambayo yataleta katika maisha yetu utukufu, afya na furaha inayofananana na ya Kristo. Maana yake ni kwamba furaha yetu na tafrija zetu zingefikia kanuni ya juu ya namna nzuri ya Kikristo. Wakati tukitambua kuwa tunazo tofauti mbalimbali za utamaduni, mavazi yetu yapaswa yawe ya kawaida, si ya anasa, ya kiasi, safi, yanayowastahili wale ambao uzuri wao wa kweli hauwi wa kujipamba kwa nje, bali kwa mapambo yasiyoharibika, yaani roho ya upole na utulivu. Pia ina maana ya kwamba kwa kuwa miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu, lazima tuitunze kwa busara. Pamoja na mazoezi ya kutosha na kupumzika yatupasa kuchagua vyakula vyenye afya kadiri inavyowezekana na kuepuka vyakula visivyo safi, vilivyo najisi, vilivyotajwa katika Maandiko Matakatifu. Kwa sababu vinywaji vya vileo, pombe, mvinyo, tembo, moshi, tumbako na matumizi mabaya ya madawa na madawa ya usingizi huleta madhara kwa miili yetu, yatupasa kuepukana nayo kabisa. Badala yake yatupasa tuyafuate yo yote yale yatkayotuletea mawazo na miile yetu iwe kamili, yenye furaha na wema.” (1Yoh.2; Efe.5:1-21; Rum.12:1, 2; 1Kor.6:19, 20; 10:31; 1Tim.2:9, 10; Wal. 11:1-47; 2Kor.6:4-7; 1Pet.3:1-4; 2Kor.4:8; Fil.4:8; 3Yoh.2)

Mwenendo wa Mkristo huja kama mwikio kushukuru wokovu mkuu aliouleta Mungu kupitia Yesu Kristo. Paulo anawaomba waumini wote “Basi ndugu zangu, nawasihia kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu na ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishie namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza kwa ukamilifu. (Rum.12:1, 2).Kwa hiyo wakristo kwa makusudi, hulinda na kukuza uwezo wao wa kiakili, kimwili na wa kiroho ili wamheshimu na kumtukua Mwumbaji na Mwokozi wao.

Kristo aliomba “siombi kwamba uwatoe katika uwatoe katika ulimwengu; bali uwalinde na yule mwovu. Wao si wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu.” (Yoh.17:15, 16). Ni muhimu kujua kwa jinsi gani wakristo wanaokaa duniani lakini wawe tofauti na ulimwengu. Kristo kielelezo chetu aliishi duniani humu akichanganyika na watu lakini hakutenda dhambi. Aliitwa mlafi na mlevi (Mt.11:19) lakini hakuna awezaye kuthibitisha kwamba alitenda dhambi (Yoh. 8:46).

Mwenendo na Wokovu

Katika kuchagua upi ni mwenendo unaofaa, twapaswa kuepuka kukithiri kwa aina mbili. Kwanza ni kuzipokea sheria na matumizi ya misingi ya afya kama njia ya wokovu. Kutaka kuhesabiwa haki kwa matendo ya mwili ni kujitenga na Kristo (Gal.5:4). Kinyume chake, kukithiri kwingine ni kutumia uhuru vibaya kwa kutenda dhambi. (Gal. 5:13). Ikiwa kila mtu atafuata aonavyo vema, hapatakuwa na kuonyana kama ilivyofundishwa na Yesu katika Mathayo sura ya 18 na Wagalatia 6:1, 2. Wakati mwenendo na hali ya kiroho vinahusiana sana, hatuwezi kuupata wokovu kwa mwenendo mwema. Wakati wokovu ni kwa njia ya Kristo peke yake, mwenendo mwema ni matokeo ya kile Yesu alichotimiza kutuokoa, pale Kalvari.

Mahekalu ya Roho Mtakatifu

Siyo Kanisa pekee bali hata mkristo mmoja mmoja hufanya hekalu la Roho Mtakatifu (1Kor.6:19). Kwa nafasi yetu kama Wakristo yatupasa kujali hali ya kiroho na kimwili ya wanadamu kama Yesu alivyojali. Twasoma kuwa aliponya “ugonjwa na udhaifu” wa kila namna (Mt.4:23). Sheria za Mungu ambazo hujumuisha sheria za afya, haziumizi bali zimewekwa na Muumbaji kutusaidia kuyafurahia maisha katika ujazo wake. (Angalia Yoh.10:10).

Baraka ya Mungu ya Afya Kamili

Kupata afya bora hutegemea kufuata kwa uaminifu kanuni zilizotolewa na Mungu. (Kut.15:26). Baadhi ya kanuni hizi ziko wazi na zinakubalika na watu wote. Kwa sababu wanadamu wana mazoea tofauti, kanuni zingine za afya huwakwaza, zikaonekana hazieleweki, zikahojiwa na hata kukataliwa.

A) Baraka ya mazoezi. Mazoezi ya kuzingatiwa daima ni kanuni ndogo iletayo nguvu, mwili imara, inaondoa msongo wa mawazo, ngozi yenye afya, kujiamini, kutawala uzito wa mwili, kusaidia uyeyushaji wa chakula mwilini na kupunguza uwezekano wa kupata magonjwa ya shinikizo la damu na magonjwa ya moyo. Mazoezi siyo jambo la uchaguzi bali ni muhimu kwa afya bora. Kazi ya manufaa huleta ustawi na uvivu hufanya mtu awe omba omba (Angalia Mith.6:6-13; 14:23). Mungu aliwapa kazi wazazi wetu wa kwanza kutunza nyumba yao kwenye uwazi. (mwa.2:5, 15; 3:19). Yesu alipokuwapo duniani aliweka kielelezo cha kufanya kazi, kwanza kwenye karakana ya seremala na pili akiwa katika huduma alitembea miji na vijiji.

B) Baraka ya mwanga wa jua. Mwanga ni muhimu kwa uhai. (Mwa.1:3). Nuru huwezesha michakato izalishayo lishe inayotupatia nguvu na kuachia hewa ya Oxygen tunayovuta. Mwanga hukuza hali ya afya na uponyaji.

C) Baraka ya maji. Asilimia sabini na tano (75%) ya miili yetu ni maji. Maji hupotea mwilini kwa njia ya kupumua, jasho na kuondosha uchafu. Ili tubaki na afya, ni muhimu kuyarejesha maji yanayopotea kwa kunywa glasi zisizopungua nane (8). Matumizi mengine ya maji ni kwa usafi na kuburudisha.

D) Baraka ya hewa safi. Mazingira yasiyo na hewa safi husababisha damu kubeba hewa ya Oxygen kidogo kuliko inavyotakiwa. Hiyo humfanya mtu asiwe mwangalifu na mwenye kuitikia kwa uzito kutekeleza yanayohitajika. Hivyo ni muhimu kujipatia hewa safi ya kutosha kila siku.

E) Baraka ya kuishi kwa kiasi, bila madawa wala vichocheo. Madawa yamejaa kwenye jamii yetu kwa sababu huchangamsha mwili na kuondoa maumivu na msongo. Wakristo tumezungukwa na vishawishi kuvitumia madawa. Hata viburudisho vingine vinavyoonekana havina matatizo huwa vina madawa. Kahawa, chai na kola vina kafeini, na vinywaji baridi vyenye ladha ya matunda huwa na vilevi. Utafiti umethibitisha kwamba matumizi ya vinywaji vyenye vilevi kidogo huongoza kwenye vinywaji vyenye vilevi vinavyoathiri akili.

1. Tumbaku. Katika umbo lolote, tumbaku ni sumu inayoua polepole yenye kuathiri mwili, akili na uwezo wa kimaadili. Mara ya kwanza athari zake huwa hazionekani. Huchangamsha kisha huhafifisha mfumo wa fahamu, ikizorotesha na kuyumbisha uwezo wa ubongo.

Wale wanaotumia tumbaku huwa wanajiua wenyewe polepole na kuvunja amri ya Mungu isemayo usiue. (Kut.20:13)

2. Vinywaji vya kulevya. Pombe (alcohol) hutumika sana duniani. Yapo mafungu ya Biblia yanashauri kutumia kidogo mvinyo. (Kumb. 33:28,) na la kushangaza, ilisemwa pia yaweza kutumika wakati wa sikukuu za ibada (Kumb.14:26). Kwenye Agano Jipya, Paulo anampa kilevi mchungaji kijana kama dawa (1Tim.5:23). Na kufundisha kuwa viongozi wa kanisa wasizoe ulevi (Tit. 1:7).

Izingatiwe kuwa pombe ineleta madhara makubwa kwenye ini na mfumo wa fahamu ikiwemo na ubongo. Kwa kuwa Mungu huwasiliana nasi kupitia ufahamu, kwa kutumia pombe, mfumo huathirika sana. Imethibitika kwamba kadiri kiwango cha pombe kinapoongeza, hali ya mtu hubadilika kutoka kukosa kuratibu mambo, kuchanganyikiwa, kutokuelewa, neva kushindwa kazi (kaput), kuzimia na hata kufa. Musa aliruhusu kutumia mvinyo, lakini kama Yesu alivyopata kuonya, mengine yaliruhusiwa kwa ugumu wa mioyo ya wanadamu tu. (Mt.19:8). Mwanzo Edeni, hatuna mahali paliporuhusiwa kutumia pombe. Kwa kuwa maarifa yaliyoko duniani yanasema kwamba ukianza kunywa kilevi, utazoelea na itakuwa vigumu kuiacha, ushauri mwema ni kwamba tuachilie mbali ulevi (1Sam. 1:14).

3. Madawa mengine na madawa ya kulevya. Yako madawa mengine hatari kwa matumizi ya mwanadamu pamoja na madawa ya kulevya ambayo Shetani hutumia kumharibu mwanadamu. Wakristo wa kweli watamtukuza Mungu kwa miili yao kwa kuwa na mali ya thamani ya Mungu ambayo imenunuliwa kwa bei kubwa. (1Kor.6:19,20).

F) Baraka ya Pumziko. Pumziko halisi ni muhimu kwa afya. Yesu anaendeleza agizo lake kwa wanafunzi waliochoka “njoni ninyi peke yenu kwa faragha, mahali pasipokuwa na watu, mkapumzike kidogo” (Mk.6:31). Nyakati za utulivu za mapumziko hutoa fursa kumtafakari Mungu “Acheni mjue ya kuwa Mimi ni Mungu” (Zab.46:10). Mungu alisisitiza hitaji la mwanadamu la pumziko kwa kuweka siku ya saba kama siku ya pumziko. (Kut.20:10). Mawazo yanayochoshwa kwa mahangaiko ya dunia, yapaswa kuelekezwa palipo na maburudiko yajengayo afya. Hivyo hatutaifuata dunia. (1Yoh.2:15, 16).

1. Sinema, televisheni, radio na video. Vifaa hivi vya mawasiliano vyaweza kuwa nyenzo za elimu. Vimegeuza ulimwengu na kufanya maisha, mawazo, matukio ya ulimwengu mzima kufikiwa kirahisi katika hali halisi. Mkristo apaswa kukumbuka kwamba vile tuonavyo, televisheni na video huathiri mtu zaidi kuliko kitu kingine chochote. Athari zake ni kubwa sana nyumbani. Yesu alionya chochote kinachokosesha, chafaa kujitenga nacho. (Mt.5:29, 30). Paulo alisema tukitazama tunabadilishwa toka utukufu hadi utukufu. (2Kor.3:18). Katika kulinda moyo (Mith. 4:23) ni vema kutafakari yanayoleta maana katika maisha, yenye kupendeza, sifa nzuri, wema nk. (Filp. 4:8).

2. Kusoma na muziki. Kanuni kama iliyotolewa kwa sinema, televisheni, radio na video itatumika kwenye muziki. Wafuasi wa Kristo hawatasoma mambo yenye mwelekeo wa uovu au kusikiliza muziki unaoshawishi kutenda dhambi. (Rum.13:11-14; 1Pet.2:11).

3. Matendo yasiyokubalika. Waadventista pia hufundisha kuwa kucheza kamari, karata, kwenda kwenye majumba ya kuigiza, na kusakata dansi vyafaa kuepukwa. (1Yoh.2:15-17). Huhoji matumizi ya wakati ambao hutumika michezo ya kuhatarisha. (Filp.4:8).

G) Baraka ya Chakula chenye Lishe. Kwa wanandoa wa awali, Mungu aliwapa chakula kinachotokana na mimea. (Mwa.1:29). Mara baada ya kuanguka dhambini, waliongezewa mboga za kondeni. (Mwa.3:18). Chakula bora ni kile kinachotokana na mimea.

1. Chakula cha asili. Biblia haikatazi kutumia kama chakula nyama ya wanyama safi. Ni busara kutumia chakula kilichowekwa na Mungu tangu awali yaani kinachotokana na mimea; lakini ikiwa ni vigumu kukipata, twapaswa kutumia chakula bora kilichopo kwenye mazingira.

2. Wanyama safi na wasio safi. Ni baada ya gharika ndipo Mungu aliporuhusu Nuhu na familia yake kutumia nyama akionya wasitumie damu. (Mwa.9:3-5). Kwa kuruhusiwa kula nyama, Nuhu angechagua chakula chake kutoka kwa wanyama safi aliogizwa na Mungu waingie saba saba safinani. (Mwa.7:2, 3). Pamoja na kuwa wanyama safi walihitajika kwa chakula, bado walitumika pia kwa kutoa kafara. (Mwa.8:20). Maelezo ya kina ya wanyama safi na wasio safi hupatikana kwenye Walawi 11 na Kumbukumbu 14. Kwa kujitenga na vyakula najisi, watu wa Mungu walidhihirisha shukrani yao kukombolewa kutoka kwenye ulimwengu ulioharibika uliowazunguka. (Law.20:24-26; Kumb. 14:2). Agano jipya halikuondoa tofauti ya wanyama safi na wasio safi. Kuna mafungu yanayotumiwa vibaya kuelezea chakula (Rum.14: 2, 14, 20, 23; Mdo.10:14, 15). Ieleweke kuwa Neno la Mungu hutakasa (Yoh. 17:17) na hivyo ruhusa ya Maandiko Matakatiifu kwenye chakula ni muhimu (1Tim. 4:4, 5; Mk. 7:19).

3. Utaratibu, urahisi na uwiano. Matengenezo ya kufaa kwenye ulaji ni jambo la kuendelea na yapaswa kuingiwa kwa akili. Hatimaye twapaswa kutumia kidogo sana, vyakula vyenye sukari na mafuta. Zaidi, twapaswa kutayarisha chakula kwa njia rahisi na kwa asili inavyowezekana ili kupata mafao stahili. Chakula kitumiwe kwa utaratibu na kwa kujali wakati. Vyakula mchanganyiko na viungo husumbua uyeyushaji wake na mazoea ya kuvitumia hutumbukiza watu kwenye matatizo ya afya.

H) Baraka ya mavazi ya Kikristo. Mungu alitengeneza mavazi ya kwanza kwa wazazi wetu (Mwa.2:25; 3:21) na hujua mahitaji yetu ya mavazi. (Mt.6:25-33). Twapaswa kuzingatia kanuni za urahisi, uadilifu, kufaa kwake, afya na uzuri wa asili tunapochagua mavazi.

1. Rahisi. Kama ilivyo kwa mambo mengine yote, mavazi ya mkristo yapaswa kuwa rahisi, yenye kumtukuza Mungu. (1Kor.10:31)

2. Uadilifu. Wakristo hawatatia doa uzuri wa tabia zao kwa mitindo ya mavazi kwa ajili ya kuridhisha tamaa ya macho. (1Yoh.2:16)

3. Kufaa na gharama nafuu. Kwa sababu ni mawakili wa siri za Mungu ((1Kor.4:1), wakristo watazingatia mavazi yawe ya kufaa na yenye gharama nafuu wakiepuka mapambo ya dhahabu, lulu au thamani kubwa. (1Tim.2:9). Mavazi ya Mkristo pia yatazingatia hali ya jinsia. (Kumb.22:5).

4. Afya. Siyo chakula tu chenye kuathiri afya. Hata mavazi yapaswa kutoa afya kwa kusitiri mwili, au kutokubana mishipa ya damu na kuathiri afya.

5. Jinsi yalivyo na uzuri wa asili. Wakristo wanaelewa onyo la kuepuka “kiburi cha uzima (1Yoh.2:16). Akirejea maua ya kondeni, Yesu alisema “hata Sulemani katika fahari yake yote, hakuvikwa kama mojawapo ya hayo.” (Mt.6:29). Hivyo alidhihirisha kwamba uzuri kwa mtazamo wa kimbingu, unatazamwa kwa neema, urahiri, usafi, na uzuri wa asili. Kujionyesha kwa namna ya kiulimwengu, kama inavyoonekana katika mitindo (fasheni) haina thamani mbele za Mungu. (1Tim. 2:9). Wakristo huongoa wasio amini siyo kwa kuigiza kile ulimwengu utendacho bali kwa kudhihirisha tofauti inayoburudisha na kuvutia. Petro alisema wenzi wa maisha wasioamini “waweza kuvutwa na mwenendo wa wake zao, pasipo lile Neno; wakiutazama mwenendo wenu safi na wa hofu. Kujipamba kwenu kusiwe kujipamba kwa nje, yaani, kusuka nywele; na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi; bali kuwe utu wa moyoni usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika; yaani, roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu. (1Pet.3:1-4)

a) Tabia huonesha uzuri wa kweli wa mtu. Wote Petro na Paulo wameweka kanuni ya kufuatwa na wanaume na wanawake wakristo kwenye eneo la mapambo. “Kujipamba kwenu kusiwe kujipamba kwa nje, yaani, kusuka nywele; na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi;” (1Pet.3:3). “Vivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi; si kwa kusuka nywele, wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za thamani; bali kwa matendo mema, kama iwapasavyo wanawake wanaoukiri uchaji wa Mungu” (1Tim.2:9, 10).

b) Urahisi unawiana na matengenezo na uamsho. Yakobo alipotoa wito kwenye familia yake kujitoa kwa Mungu, walimpa “miungu migeni yote iliyokuwa mikononi mwao, na pete zilizokuwa masikioni mwao, naye Yakobo akazificha chini ya mwaloni ulioko Shekemu” (Mwa.35:2, 4). Baada ya Waisraeli kwa ndama wa dhahabu, Mungu aliamuru “basi sasa vueni vyombo vyenu vya uzuri ili nipate kujua nitakalowatenda.” Kwa kutubu “wakavua vyombo vyao vyote vya uzuru, tangu mlima wa Horebu na mbele.” Paulo kwa uwazi anasema kuwa kumbukumbu hii iliwekwa ili kutuonya sisi tuliofikiwa na miisho ya zamani. (1Kor.10:11).

c) Uwakili mwema unahitaji maisha ya kujinyima. Wakati sehemu kubwa ya walimwengu hawana chakula, uyakinifu (materialism) unawatengea wakristo majaribu kuanzia kuwa na mavazi ya gharama, magari, mapambo na nyumba za fahari. Unyenyekevu katika maisha na mwonekano unawatenga wakristo kinyume na uchoyo, uyakinifu, majigambo ya kipagani, jamii ya karne ya 21, mahali ambako thamani huwekwa kwenye vitu badala ya kwa watu.

Biblia hukemea mapambo yasiyo ya asili na huyahusisha na upagani na uasi (2Waf. 9:30, Yer.4:30). Kuhusiana na mapambo, wakristo wapaswa kuwa na mwonekano wa asili. Ikiwa tutamwinua Mwokozi katika namna tunavyosema, tunavyotenda na tunavyovaa, tutakuwa sumaku tukiwavuta watu kwake. “Katika nchi nyingine desturi ya kuvaa pete ya ndoa huchukuliwa kuwa lazima, baada ya kuingia mawazoni mwa watu kuwa ni kipimo cha maadili mema, na hivyo haichukuliwi kuwa pambo. Katika hali ya namna hiyo Waadventista wa Sabato hawana nia ya kulaumu desturi hiyo.” (Angalia Mwongozo wa Kanisa).

Kanuni za Viwango vya Kikristo

Katika kujifunua kwake kote, mtindo wa maisha wa mkristo ni mwitikio wa wokovu unaopatikana kwa njia ya Kristo. Mkristo ananua kumheshimu Mungu na kuishi kwa namna ambayo Yesu angeliishi.

Wakati wengine wanaweza kuwa na mtazamo kuwa kanuni za maisha ya kikristo zimejaa makatazo, twapaswa kuzitazama kanuni chanya katika katika mhimili wa wokovu. Roho Mtakatifu anapokuwa amefanya maskani kwenye moyo wa mtu, mabadiliko yanayotokea kumzunguka mtu huyo ni makubwa na yataonekana kwa wanaomzunguka. (Yoh. 3:8). Roho si kwamba hufanya mabadiliko katika moyo bali pia huendeleza kutenda kazi kwake kwa mkristo. Tunda la Roho ni upendo (Gal.5:22, 23). Hoja yenye nguvu ya ubora wa ukristo ni mkristo anayependa na kupendeka.

Kuishi na Nia ya Kristo. “Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yeu” (Filp. 2:5). Katika mazingira yanayofaa au yasiyofaa, twapaswa kuelewa na kuishi sawa sawa na nia ya Kristo (1Kor.2:16). Utii wa kweli huanzia moyoni. Moyo ukipenda kufanya kazi na Yesu, na tukiridhia, Kristo atajitambulisha kwenye mawazo yetu na makusudi na hivyo kuunganisha nia zetu na nia yake. Kwa kuithamini tabia ya Kristo mioyoni mwetu na mawasiliano ya kudumu na Mungu, dhambi itakuwa kitu cha kuchukiza.

Kuishi Tukimsifu na Kumtukuza Mungu. Mungu ametutendea mengi sana. Njia mojawapo tunayoweza kuonyesha shukrani zetu kwake ni kwa kumsifu. Zaburi hukazia jambo hili la kiroho. “Ndivyo nilivyokutazama katika patakatifu, nizione nguvu zako na utukufu wako, Maana fadhili zako ni njema kuliko uhai; midomo yangu itakusifu. Ndivyo nitakavyokubariki maadamu ni hai; Kwa Jina lako nitaiinua mikono yangu. Nafsi yangu itakinai kama kushiba mafuta na vinono; Kinywa changu kitakusifu kwa midomo ya furaha. (Zab. 63:2-5).

Kwa mkristo mtazamo huo wa sifa utahifadhi mambo mengine ya kiroho katika mtazamo unaofaa. Kwa kumtazama Mwokozi aliyesulubiwa aliyetukomboza kutoka adhabu ya dhambi na mamlaka ya dhambi, tunavutwa kuzishika amri zake “na kuyatenda yapendezayo machoni pake.” (1Yoh.3:22 cf. Efe.5:10). Wakristo hawako “hai tena kwa ajili ya nafsi zao wenyewe, bali kwa ajili yake yeye aliyekufa akafufuka kwa ajili yao” (1Kor.5:15). Kila aliye mkristo wa kweli atamweka Mungu kwanza katika yote atendayo, afikiriyo, asemayo na yote anayotamani. Hana Mungu mwingine mbele za Mkombozi. (1Kor.10:31).

Kuishi kuwa Mfano. Paulo alionya msikoseshe yeyote (1Kor.10:32). Alijizoeza asiwe na dhamiri isiyo na hatia mbele za Mungu na mbele za watu siku zote. (Mdo.24:16). Tukikosesha tunakuwa kwazo kwa wale ambao Yesu aliwafia. (Luk.17:1, 2). Anayekaa ndani yake “imempasa kuenenda mwenyewe vile vile kama yeye alivyoenenda” (1Yoh.2:6).

Kuishi ili Kutumika. Sababu kubwa inayowafanya wakristo waishi kama waishivyo ni kuokoa wanaume na wanawake waliopotea. Paulo alisema anajitahidi kuwapendeza watu wote “nisitake faida yangu mwenyewe, ila faida yao walio wengi, wapate kuokolewa.” (1Kor.10:33; cf. Mt.20:28).

Masharti na Mwongozo.

Katika Kanuni za Kanisa, yamewekwa masharti juu ya kutotumia tumbaku, bangi, madawa na madawa ya kulevya, pombe, vyakula najisi. Haya ni mahitaji kidogo kwa mkristo anayekuwa. Hatupaswi kuhukumu wanaojaribiwa (Rum.14:1; 15:1). Kanuni njema ni kutenda yote kwa utukufu wa Mungu (1Kor.10:31).